# HALMASHAURI YA WILAYA YA KONDOA
## MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO KILICHOFANYIKA TAREHE 24/01/2022 KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA HALMASHAURI - BUKULU

**WALIOHUDHURIA:**

**A. MADIWANI**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Abdallah S. Maguo | Diwani/Mnenia | - | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Madina M. Mrimi | Diwani/Busi | - | Mjumbe |
| 3. | Mhe. Rahim H. Salum | Diwani/Salanka | - | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Abubakari S. Maleda | Diwani/Kisese | - | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Msimbira M. Mcharia | Diwani/Itololo | - | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Amina I. Msepwa | Diwani/V Maalumu | - | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Ngware S. Ngware | Diwani/Kikore | - | Mjumbe |
| 8. | Mashauri M. Vicent | Kaimu Mkurugenzi Mtendaji (W) | | Katibu |

**B: WASIOHUDHURIA KWA TAARIFA**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Dr. Ashatu Kijaji | Mbunge Jimbo la Kondoa |
| 2. | Mhe. Zamdini M. Hamis | Diwani/Itaswi |

**C: WAKUU WA IDARA**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Andrea I. Ng'hwani | Katibu Tawala (W) |
| 2. | Philbert Prosper | Kaimu Mkuu wa Idara ya Utawala na Utumishi |
| 3. | Gasper A. Temu | Kny; Mkuu wa Idara ya Mifugo na Uvuvi |
| 4. | Joshua S. Mnyang'ali | Mkuu wa Idara ya Mipango |
| 5. | Rahiya Nasser | Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii |
| 6. | Qs. Felchismi Tesha | Kaimu Mkuu wa Idara ya Ujenzi |
| 7. | Njenjela Ally | Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani |
| 8. | Kassim N. Herra | Mkuu wa Idara ya Fedha |
| 9. | Hamis B. Rajabu | Kny; Mkuu wa Idara ya Elimu Msingi |
| 10. | Heri H. Suba | Kny; Mkuu Kitengo cha TEHAMA |
| 11. | Deogratius Michael | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Nyuki |
| 12. | Emmanuel L. Mvungi | Kny; Mkuu wa Idara ya Ardhi na Maliasili |



Scanned with CamScanner

| | |
|---|---|
| 13. Samwel Mseselo | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi |
| 14. Dr. Nelson Kimolo | Mkuu wa Idara ya Afya |
| 15. Paul S. Lubuva | Kny; Mkuu wa Kitengo cha Mazingira na Takangumu |
| 16. Donald S. Jidayi | Mratibu wa TASAF |

Scanned with CamScanner

**MUHT.NA.01/2021/2022KUFUNGUA KIKAO**

Mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe katika kikao kisha kufungua kikao mnamo saa 03:57 asubuhi baada ya kutimia kwaakidi lazimu ya wajumbe.

**MUHT.NA.02/2021/2022**

Agenda zifuatazo zilithibitishwa kuwa agenda za kikao ambapo agenda mbili ziliongezwa,Na. 8.Maombi ya Mhe. Mkuu wa Wilaya ya Kondoa kuhamishia Ofisi yake kwenye Ofisi za zamani za Mkurugenzi Mtendaji (W) Kondoa na agenda Na. 9. Masuala yaKiutumishi.

1. Kufungua kikao
2. Kuthibitisha agenda za kikao
3. Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa kikao cha kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango cha tarehe 06/01/2022
4. Yatokanayo na muhtasari wa kikao cha kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango cha tarehe 06/01/2022
5. Taarifa ya Mapato na Matumizi katika kipindi cha mwezi Desemba, 2021
6. Kupokea na kujadili taarifa za utekelezaji shughuli kutoka katika Idara mbalimbali kwa kipindi cha robo ya pili (Oktoba – Desemba), 2021/2022
   - Kitengo cha Manunuzi
   - Idara ya Utumishi na Utawala
   - Kitengo cha Sheria
   - Idara ya Mipango
   - Kitengo cha TEHAMA
7. Mapendekezo ya Vikundi vitakavyopewa mikopo katika kipindi cha robo ya pili (Oktoba – Desemba), 2021/2022
8. Maombi ya Mhe. Mkuu wa Wilaya ya Kondoa kuhamishia Ofisi yake kwenye Ofisi za zamani za Mkurugenzi Mtendaji (W) Kondoa
9. Masuala ya Kiutumishi
10. Kufunga kikao



Scanned with CamScanner

**MUHT.NA.03/2021/2022 KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO CHA TAREHE 06/01/2022**

Baada ya kuwasilishwa kwa muhtasari, kamati ilifanya marekebisho/masahihisho kadhaa kama ifuatavyo;-

Ukurasa Na. 8 wa Muhtasari, kuhusu Mabadiliko ya Tozo ya Vibali vya kuuza Mifugo minadani. Kamati ilijadili kwa kina ambapo iliona kwamba wananchi watakuwa wanayumbishwa hivyo iliridhia Halmashauri iendelee kutoza viwango vipya vilivyowasilishwa katika kikao hadi pale mchakato wa kutunga Sheria mpya za ushuru wa mazao na mifugo utakapokamilika.

Baada ya masahihisho hayo kufanyika, kamati iliridhia kusainiwa kwa muhtasari huo ili iwe kumbukumbu sahihi za kikao.

**MUHT.NA.04/2021/2022 YATOKANAYO NA MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO CHA TAREHE 06/01/2022**

Taarifa ya utekelezaji wa maazimio/maagizo ya kikao kilichopita iliwasilishwa ikionesha namna ambavyo maagizo hayo yalitekelezwa na wahusika ambapo katika yatokanayo Na. 3 Kuhusu vitambulisho vya Wazee, kamati ilihoji ili kujua mpango uliowekwa kuhakikisha wazee wote 6,000 waliobakia wanapata vitambulisho.

Ufafanuzi ulitolewa kwamba, kwa kuwa Halmashauri imepokea fedha za Mfuko wa pamoja wa Afya (Health Sector Basketi Fund), Halmashauri itahakikisha wazee wote wanapatiwa vitambulisho kabla ya mwaka wa fedha 2021/2022 kumalizika.

Aidha, kwa sasa huduma za matibabu kwa wazee wasiokuwa na vitambulisho zinaendelea kutolewa ambapo pindi wazee hao wanapopata changamoto za kiafya, hupatiwa huduma katika zahanati na vituo vya afya kupitia vibali maalum vya msamaha wa matibabu kwa wazee vinavyotolewa na Watendaji wa Vijiji na Kata.

Yatokanayo Na. 6 kuhusu Ndg. Mashaka kuendelea kuonekana kwenye Minada kama vile Salare. Kamati ilihoji juu ya kuendelea kuonekana katika maeneo ya minada Ndg. Mashaka ambapo ufafanuzi ulitolewa kuwa Ndg. Mashaka alikwisha simamishwa katika shughuli zozote za ukusanyaji Mapato ya Halmashauri minadani ambapo sambamba na hilo, Halmashauri haikuwahi kuwa na mkataba wowote wa ukusanyaji mapato na Ndg. Mashaka hivyo kuendelea kuwepo kwake minadani huenda akawa anafanya shughuli zake binafsi.



Scanned with CamScanner

**Azimio/Agizo**

Kamati iliagiza kuwa Halmashauri ijiridhishe juu ya uwepo wa Ndg. Mashaka katika maeneo ya minada akishiriki kufanya shughuli za ukusanyaji mapato ya Halmashauri.

**MUHT.NA.05/2021/2022 TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI MWEZI DESEMBA, 2021/2022**

Kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022 Halmashauri ilikasimia kukusanya na kutumia jumla ya Tshs **29,011,661,978.00** ili kutekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| ➢ Vyanzo vya Ndani | Tshs | 1,570,330.901.00 |
| ➢ Ruzuku ya mishahara | Tshs | 13,471,895,652.00 |
| ➢ Ruzuku ya Utawala OC | Tshs | 580,398,000.00 |
| ➢ Ruzuku ya Utawala Idara Nyingine OC | Tshs | 1,033,492,000.00 |
| ➢ Ruzuku ya Matumizi Mengineyo OC | Tshs | 1,622,804,500.00 |
| ➢ Ruzuku ya Miradi ya Maendeleo | Tshs | 10,732,740,925.00 |
| **JUMLA** | **Tshs** | **29,011,661,978.00** |

**A. MAPATO**

Taarifa ya Mapato iliwasilishwa ikionesha kuwa kwa kipindi cha mwezi Julai hadi Desemba 2021 Halmashauri ilikusanya Jumla ya Tshs **14,552,225,085.00** sawa na asilimia **50** ya makisio ya mwaka wa fedha 2021/2022 ambapo mchanganuo wake kwa muhtasari ulikuwa kama ifuatavyo :-

| CHANZO | MAKISIO (Tshs) | MAKUSANYO | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| Vyanzo vya Ndani | 1,570,330.901.00 | 752,727,532.00 | 48 |
| Ruzuku ya mishahara | 13,471,895,652.00 | 6,541,063,600.00 | 49 |
| Ruzuku ya Utawala OC | 580,398,000.00 | 152,061,502.00 | 26 |
| Ruzuku ya Utawala Idara Nyingine | 1,033,492,000.00 | 365,593,110.00 | 35 |
| Ruzuku ya Matumizi Mengineyo OC | 1,622,804,500.00 | 1,195,507,758.00 | 74 |
| Ruzuku ya Miradi ya Maendeleo | 10,732,740,925.00 | 5,545,271,582.00 | 52 |
| **JUMLA** | **29,011,661,978.00** | **14,552,225,085.00** | **50** |



Scanned with CamScanner

## B. MATUMIZI

Kwa upande wa Matumizi, taarifa iliwasilishwa ikionesha kuwa kwa kipindi cha mwezi Julai hadi Desemba 2021Halmashauri ilitumia jumla ya Tshs **11,509,025,786.00**ambayo ni sawa na asilimia **40** ya makisio ya mwaka wa fedha 2021/2022. Mchanganuo wake kwa muhtasari ulikuwa kama ifuatavyo :-

| CHANZO | MAKISIO (Tshs) | MATUMIZI | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| Vyanzo vya Ndani | 1,570,330,901.00 | 480,102,355.00 | 31 |
| Ruzuku ya mishahara | 13,471,895,652.00 | 6,539,769,784.00 | 49 |
| Ruzuku ya Utawala OC | 580,398,000.00 | 108,451,000.00 | 20 |
| Ruzuku ya Utawala Idara Nyingine | 1,033,492,000.00 | 147,556,616.00 | 14 |
| Ruzuku ya Matumizi Mengineyo OC | 1,622,804,500.00 | 968,151,179.00 | 60 |
| Ruzuku ya Miradi ya Maendeleo | 10,732,740,925.00 | 3,264,994,851.00 | 30 |
| **JUMLA** | **29,011,661,978.00** | **11,509,025,786.00** | **40** |

Baada ya kuwasilishwa kwa taarifa ya Mapato na Matumizi kwa kipindi cha mwezi Desemba, 2021/2022 kamati ilihoji juu ya masuala kadhaa yaliyowasilishwa kwenye taarifa kisha kupatiwa ufafanuzi kama ifuatavyo;-

Katika ukurasa Na. 2 wa taarifa ya fedha, kuhusu ushuru wa majengo, kamati ilihoji ili kujua endapo Halmashauri inakusanya ushuru wa majengo kama ilivyoonekana kwenye taarifa iliyowasilishwa ambapo ufafanuzi ulitolewa kwamba kifungu hicho kinachosomeka "ushuru wa majengo" kimechajiwa hapo kimakosa badala yake kinatakiwa kisomeke "kodi ya pango".

Aidha mawasiliano na TAMISEMI yatafanyika ili kufanya marekebisho ya kifungu hiki.

Kamati ilitaka kujua kuhusu kutoonekana kwenye taarifa fedha za mauzo ya viwanja vinavyoendelea kupimwa na kuuzwa ambapo ufafanuzi ulitolewa kuwa kwa sasa kinachofanyika Bukulu ni upimaji shirikishi (Urasimishaji) ambapo kwa mujibu wa mwongozo ni kwamba zoezi hilo huendeshwa kwa kutumia kamati hivyo fedha hizo zipo chini ya kamati ya Urasimishaji. Halmashauri bado haijaanza kuuza viwanja.

Scanned with CamScanner

Baada ya majadiliano, kamati ilipokea na kuridhia taarifa ya Mapato na Matumizi iliyowasilishwa.

**MUHT.NA.06/2021/2022 KUPOKEA NA KUJADILI TAARIFA ZA UTEKELEZAJI SHUGHULI KUTOKA KATIKA IDARA MBALIMBALI KWA KIPINDI CHA ROBO YA PILI (OKTOBA – DESEMBA), 2021/2022**

- **KITENGO CHA MANUNUZI**

Iliwasilishwa tarifa ya Kitengo cha Manunuzi ikionesha shughuli zilizofanywa kwa kipindi cha robo ya pili (Oktoba – Desemba), 2021/2022 yenye sehemu mbili ambazo ni;-

i. Taarifa ya manunuzi robo ya pili.
ii. Taarifa ya stoo.

Taarifa ilionesha kuwa, Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa kwa kipindi cha robo ya pili ya mwaka wa fedha 2021/2022 ilifanya ununuzi wa jumla ya thamani ya **T.Shs 1,458,006,820.00** ikiwa ni Ununuzi wa bidhaa na huduma.

**Kuhusu utaratibu wa kutafuta wazabuni katika miradi ya ujenzi ya UVIKO 19**

Kamati ilitaka kujua kuhusu utaratibu uliotumika kutafuta wazabuni ambapo ilionekana kama mzabuni mmoja alipata zabuni ya mbao kwa shule nyingi zaidi.

Ufafanuzi ulitolewa kuwa manunuzi yote katika miradi ya ujenzi wa madarasa ya UVIKO 19 yalizingatia sheria, taratibu, miongozo na kanuni zote za manunuzi ya Umma ambapo kila shule ilifanya ununuzi wa vifaa kwa kuzingatia taratibu za manunuzi ambazo zinampa fursa mzabuni mwenye uwezo wa kusambaza vifaa vinavyohitajika kwa gharama nafuu na kwa kuzingatia ubora. Hivyo kupatikana kwa mzabuni mmoja ambae alisambaza mbao kwa shule zote kulitokana na gharama zake kuwa chini ukilinganisha na wasambazaji wengine, lakini hapakuwa na maagizo yoyote kutoka Halmashauri juu ya upatikanaji wa mzabuni mmoja aliyesambaza mbao katika shule zote zilizokuwa zinatekeleza miradi ya ujenzi wa madarasa ya UVIKO 19.

Baada ya majadiliano, kamati iliridhia na kupokea taarifa iliyowasilishwa.

Scanned with CamScanner

- **IDARA YA UTUMISHI NA UTAWALA**

Taarifa iliyowasilishwa ilionesha kuwakatika kipindi cha robo ya pili (Oktoba-Desemba), 2021/2022Idara ya Utumishi na Utawala ilitekeleza majukumu mbalimbali kama ifuatavyo:-

1. Kuidhinisha likizo za Watumishi.
2. Kuwapokea Watumishi wanaohamia
3. Kushughulikia madai ya mapunjo ya mishahara.
4. Kushughulikia bima za afya (NHIF) kwa watumishi
5. Kukusanya taarifa za ufanyikaji vikao vya kisheria kwa kipindi cha Oktoba - Disemba, 2021
6. Kuandaa vibali vya kustaafu
7. Kuwapokea ajira mpya na kuwaajiri
8. Kusimamia masuala ya Sheria, Kanuni, Taratibu za Utumishi wa Umma

Baada ya kuwasilishwa kwa taarifa kutoka katika Idara ya Utawala na Utumishi, kamati ilijadili kisha kutoa maamuzi katika masuala mbalimbali yaliyowasilishwa kama ifuatavyo;-

**Kuhusu tatizo la upungufu wa Watumishi katika kada mbalimbali**

Kamati iliagiza kuwa katika kila kikao iwasilishwe taarifa inayoonesha hatua zinazochukuliwa katika kukabiliana na upungufu wa Watumishi wa kada mbalimbali.

**Kuhusu baadhi ya Vijiji kutokuwa na akaunti hai Benki**

Kamati ilieleza kuwa vijiji vingi havina akaunti Benki hali inayopelekea Watendaji wa Vijiji kukaa na fedha nyingi mikononi na hatimae kuzitumia ambapo ufafanuzi ulitolewa kuwa kwa mujibu wa sheria ya fedha, kila kijiji kinatakiwa kuwa na akaunti Benki ambapo katika Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa, vijiji vichache ndio havijahuisha akaunti zao Benki.

**Agizo**

Kamati iliagiza kuwa Halmashauri ifanye uhakiki ili kujua kama kila kijiji kina akaunti hai Benki na vile ambavyo akaunti zao zimekuwa mfu, zihuishwe.

Baada ya majadiliano, kamati iliridhia na kupokea taarifa iliyowasilishwa.

Scanned with CamScanner

- **KITENGO CHA SHERIA**

Taarifa iliyowasilishwa ilionesha kuwakatika kipindi cha robo ya pili (Oktoba-Desemba), 2021/2022 kitengo cha Sheria kilitekeleza majukumu mbalimbali kama ifuatavyo:-

a) Kuendesha na/au Kusimamia Kesi za Halmashauri Mahakamani.

b) Kuandaa Rasimu za Sheria Ndogo za Halmashauri

c) Kutoa Ushauri wa Kisheria na Kusimamia Mabaraza ya Kata.

d) Kushirikiana na Idara/Vitengo katika Kutekeleza Majukumu

Baada ya kuwasilishwa kwa taarifa, kamati ilipongeza utendaji kazi wa Mwanasheria wa Halmashauri ambapo iliagiza kuwa kitengo cha sheria kiwe kinaonesha katika taarifa idadi ya kesi zilizopo kwenye Halmashauri za Vijiji kwa maana ya idadi ya Halmashauri zilizo shtaki/kushtakiwa.

Aidha taarifa ilitolewa kuwa kwa sasa mashauri ya ndoa na ardhi hayaruhusiwi kusikilizwa kwenye Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Kata hivyo mamlaka hayo yamehamishiwa kwenye Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya.
kamati iliridhia na kupokea taarifa iliyowasilishwa.

- **IDARA YA MIPANGO**

Iliwasilishwa taarifa ya utekelezaji shughuli katika kipindi cha robo ya pili (Oktoba – Desemba), 2021/2022 ambapo taarifa hiyo ilionesha kuwa katika mwaka wa fedha 2021/2022 Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa imeidhinishiwa kukusanya na kutumia jumla ya**Tshs. 13,558,942,102.60** kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo kutokana na vyanzo mbalimbali vya mapato (Mapato ya Ndani, Ruzuku kutoka Serikalini na fedha za Wahisani/Wadau wa Maendeleo wa ndani na nje ya nchi) ikijumuisha fedha za salio anzia **Tshs. 2,342,201,178.00**na fedha idhinishwa kiasi cha **Tshs. 11,216,740,925.00**

Aidha,katika kipindi cha Oktoba – Desemba, 2021/2022 Halmashauri ilipokea kiasi cha **Tshs.5,245,001,143.00** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ambapo jumla ya **Tshs. 3,125,132,146.00** zilikuwa zimetumika ikiwa ni sawa na asilimia 43 ya fedha zilizokuwepo katika kipindi hicho



Scanned with CamScanner

Fedha hizi zilizopokelewa kiasi cha **Tshs.5,245,001,143.00** na zilizokuwepo kama salio anzia kutoka robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2021/2022 kiasi cha **Tshs.2,027,534,626.00** zimeendelea kutumika kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa miundombinu katika sekta za Elimu Msingi, Elimu Sekondari, Afya na Utawala.

Baada ya kuwasilishwa taarifa ya utekelezaji kazi kutoka katika Idara ya Mipango, ilipokelewa na kuridhiwa.

- **KITENGO CHA TEHAMA**

Taarifa iliyowasilishwa ilionesha kuwakatika kipindi cha robo ya pili (Oktoba-Desemba), 2021/2022 kitengo cha TEHAMA kilitekeleza majukumu mbalimbali kama ifuatavyo:-

1. Uandaaji wa 'Server' kwa ajili ya mfumo wa GoT-HoMIS zahanati ya Mkekena,Chololo,Thawi,Kiteo na Chubi.
2. Kufanya maboresho ya matumizi ya mfumo wa GoT-HoMIS Toleo na.3 katika kituo cha afya Busi.
3. Uwezeshaji wa matumizi ya mfumo wa FFARS kwa watumiaji wa shule ya sekondari ya Changaa,kwadelo,Intela na Thawi.
4. Utoaji mafunzo ya Uandikishaji na uhuishaji wanachama wa Mfuko wa bima ya Afya CHF kwa waandikishaji kwa kutumia toleo jipya linalohusisha mfumo wa GePG.
5. Kuendelea kusimamia na kuwezesha watumiaji wa mfumo wa mapato LGRCIS kufanya kazi katika mfumo kwa ufanisi.
6. Kuendelea kuwezesha Idara ya Utumishi na Utawala kutekeleza majukumu yao kwa kutumia mifumo na vifaa walivyonavyo.
7. Kuendelea kutoa taarifa mbalimbali kwa jamii kupitia Tovuti ya Halmashauri.

Baada ya kuwasilishwa taarifa ya utendajii kazi ya kitengo cha TEHAMA ilipokelewa na kuridhiwa na kamati.

**MUHT.NA.07/2021/2022 MAPENDEKEZO YA VIKUNDI VITAKAVYOPEWA MIKOPO KATIKA KIPINDI CHA ROBO YA PILI (OKTOBA – DESEMBA), 2021/2022**

Iliwasilishwa taarifa iliyoonesha orodha ya vikundi vitatu (3) kutoka katika makundi ya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu vilivyokidhi vigezo na kupendekezwa



Scanned with CamScanner

kupatiwa mikopo yenye thamani ya **Tshs. 46,710,000.00** kama mchanganuo unavyoonekana hapo chini;-

| NA | JINA LA KIKUNDI | AINA YA KIKUNDI | KATA/KIJIJI | SHUGHULI | KIASI KILICHOOMBWA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | ITONGWI YOUTH GROUP | VIJANA | KALAMBA CHINI | USEREMALA | 11,000,000.00 |
| 2 | IDINDIRI GROUP | WANAWAKE | KEIKEI – IDINDIRI | UFUGAJI NYUKI | 10,710,000.00 |
| 3 | KIKUNDI CHA HABARI NJEMA | WATU WENYE ULEMAVU | ITASWI – KISAKI | KIWANDA KIDOGO CHA MAFUTA YA ALIZETI | 25,000,000.00 |
| **JUMLA KUU** | | | | | **46,710,000.00** |

Baada ya kuwasilishwa kwa mapendekezo ya vikundi vitakavyopatiwa mikopo, kamati ilihoji kuhusu sababu zinazopelekea ucheleweshwaji wa utoaji wa mikopo kwa wakati kwa vikundi vilivyoidhinishwa kupatiwa mikopo hiyo ambapo ufafanuzi ulitolewa kwamba, ni kweli kulikuwa na changamoto za kibenki katika benki ya CRDB kwa kipindi kirefu lakini changamoto hiyo imekwisha shughulikiwa ambapo hadi tarehe 24/01/2022 vikundi vyote vilivyoidhinishwa vimekwishapatiwa mikopo.

**MUHT.NA.08/2021/2022 MAOMBI YA MHE. MKUU WA WILAYA YA KONDOA KUHAMISHIA OFISI YAKE KWENYE OFISI ZA ZAMANI ZA MKURUGENZI MTENDAJI (W) KONDOA**

Baada ya kuwasilishwa kwa barua yenye **Kumb. Na. AB/233/304/01/115** ya tarehe **18/01/2022**kutoka katika Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Kondoa iliyolenga kuomba kuhamishia Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Kondoa kwenye Ofisi za zamani za Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri (W) Kondoa, kamati ilipokea na kuridhia maombi hayo kwamba Mhe. Mkuu wa Wilaya ya Kondoa apewe vyumba hivyo kama alivyoomba.

**MUHT.NA.09/2021/2022 MASUALA YA KIUTUMISHI**

Iliwasilishwa agenda inayohusua masuala ya Kiutumishi ambapo masuala yanayohusu Watumishi yalijadiwa. Aidha, wataalam walitolewa nje kisha Katibu wa kikao, Afisa Utumishi pamoja na Waheshimiwa Madiwani wa kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango walibakia ukumbini ili kujadili agenda hii.



Scanned with CamScanner

**MUHT.NA.10/2021/2022 KUFUNGA KIKAO**

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa ushiriki wao katika majadiliano kishakufunga kikao mnamo saa 06.08 Mchana.

**MUHTASARIUMETHIBITISHWA**

............................ ............................

**KATIBU** **MWENYEKITI**

**TAREHE** ..........................



Scanned with CamScanner